# Bibilia ya watoto
## Inawaletea

# Kwaheri Farao!

Kimeandikwa na: Edward Hughes
Kimeorodheshwa na: Janie Forest
Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home
Imerekebishwa na: Lyn Doerksen



Hadithi 11 baadhi ya 60

**www.M1914.org**

***Bible for Children,*** *PO Box 3, Winnipeg, MB R3C 2G1 Canada*


Leseni: Unahaki ya kunakili au kuchapisha hadithi hii. Mradi tu.

Kiswahili Swahili



Wasimamizi wakawapiga baadhi ya watumwa kwasababu hawakuwa na muda wa kukusanya majani na bado wafyatue

matofali ya kutosha.



3

Watu wakawalaumu Musa na Haruni kwa kuwaletea matatizo. Musa akapata mahali pa kuomba. Akalia akisema, "Ee BWANA, hujawaokoa watu wako hata kidogo."

Mungu akajibu, "Mimi ni BWANA, na nitawatoa Misri."

4

Kisha Mungu akamtuma Musa na Haruni tena kwa Farao. Mtawala mkuu alipowauliza watumishi wa Mungu kuhusu ishara kutoka

kwa Mungu, fimbo ya Haruni ikageuka nyoka anayetambaa.

5

Farao akasema kwa ukali, "Waiteni wachawi wangu." Wachawi wa Kimisri walipotupa fimbo zao, kila fimbo ikawa nyoka pia. Lakini fimbo ya Haruni ikazimeza. Bado Farao akakataa kuwaruhusu waondoke.

6

Asubuhi iliyofuata, Musa na Haruni wakakutana na Farao mtoni. Haruni aliponyosha fimbo yake, Mungu akageuza maji kuwa damu. Samaki wakafa! Watu hawakuweza kuyanywa!



7

Lakini Farao akaufanya moyo wake kuwa mgumu. Hakuwaruhusu Waisraeli kuondoka Misri.



8

Kwa mara nyingine, Musa akamwambia Farao awaruhusu watu wa Mungu waondoke. Farao akakataa tena. Mungu akatuma pigo jingine. Misri yote ikajaa vyura. Kila nyumba, kila chumba, hata majiko ya kupikia yalifurika vyura!

9

Farao akawasihi, "Niombeeni, ili Mungu awaondoe vyura ndipo nitaruhusu watu wenu waondoke." Lakini vyura walipoondolewa, Farao akabadili nia yake. Hakuwaachia huru watumwa.

10

Kisha Mungu akatuma mabilioni ya chawa. Kila mtu na mnyama aliwashwa kwa kuumwa na chawa hao, lakini bado Farao hakukubaliana na mpango wa Mungu.

11

Baada ya hapo, Mungu akatuma makundi ya inzi. Mungu akatuma magonjwa kuua mifugo ya Wamisri.

12

Mungu akatuma majipu yanayouma sana. Watu wakateseka sana. Bado Farao akampinga Mungu.

13



Baada ya pigo la majipu, Mungu akatuma makundi ya nzige. Nzige wakala kila jani la mmea katika nchi.

14

Kisha Mungu akatuma siku tatu za giza nene. Lakini Farao mwenye moyo mgumu hakuwaachia huru Waisraeli.

15

Mungu akaonya, "Nitatuma pigo jingine moja. Usiku wa manane, wazaliwa wote wa kwanza wa wanadamu na wanyama watakufa." Mungu akawaambia Waisraeli kwamba wazaliwa wao wa kwanza wataokolewa kama watapaka damu ya mwanakondoo kwenye miimo ya milango yao.



16

Usiku wa manane, kilio kikuu kikatokea Misri. Mauti iliwapiga. Katika kila nyumba alikufa mtu mmoja au zaidi.

17



Farao akamuomba Musa akisema, "Ondokeni muende kumtumikia BWANA." Mara watu wa Mungu wakatoka katika mipaka ya Misri.

18



Mungu akamwambia Musa kuhusu kukumbuka usiku wa Pasaka kwasababu malaika wa Mungu alipita juu ya nyumba za Waisraeli na kumpiga Farao na watu wake.

19



Baada kukaa miaka 430 Misri, watu wa Mungu walikuwa sasa wako huru. Mungu akawaongoza kwa nguzo ya wingu mchana na nguzo ya moto usiku.

20

Lakini Farao alikuwa hajaridhika kuwaachia Waisareli. Akamsahau tena Mungu. Akabadili nia yake tena. Akakusanya jeshi lake na kuwafukuzia watumwa. Mara akawanasa kati ya mwamba na bahari.

21

Musa akawaambia, "Mungu atawapigania." Musa akauendea ukingo wa maji na kunyosha mkono wake.

22



Muujiza mkubwa ukatokea. Mungu akafungua njia kwenye maji. Watu wakavuka salama.

23

Kisha jeshi la Farao likakimbilia ndani ya bahari ya shamu. Maaskari wakafikiri, "Sasa tutawakamata."

24

Lakini Mungu akayafunga maji. Jeshi hodari la Misri likamezwa. Ndipo Farao akajua kwamba Mungu wa Israeli ni BWANA juu ya yote.



25

Kwaheri Farao!

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Kutoka 4-15

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."
Zaburi 119:130

**Mungu anajua** kuwa tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Mshahara wa dhambi ni mauti.

**Mungu anatupenda** sana hadi akamtuma mwana wake, Yesu, aje afe msalabani na alipe mshahara ule wa dhambi. **Yesu alifufuka** na akarudi mbinguni! Sasa Mungu anaweza kusamehe dhambi zetu.

**Kama unataka kuondoka kwa dhambi zako,** mwambie Mungu haya: Mungu mpendwa, ninaamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili yangu na anishi tena. Tafadhali njoo maishani mwangu na usamehe dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya na niwe nawe milele. Nisaidie niishi kwako kama mtoto wako. Yohana 3:16

**Soma bibilia na zungumza na Mungu kila siku!**